**RIPOTI YA TATHMINI YA CAO**

**Kuhusu Masuala yanayohusiana na**

**Uwekezaji wa IFC kwa shule za Bridge International Academies (#32171) nchini Kenya**

Juni 2019

Afisi ya Compliance Advisor Ombudsman
*kwa niaba ya*
Shirika la Fedha la Kimataifa na
Wakala wa Dhamana ya Uwekezaji wa Wahusika Anuwai
**www.cao-ombudsman.org**

## Kuhusu CAO

Afisi ya Compliance Advisor Ombudsman (CAO) ni utaratibu wa uwajibikaji unaojisimamia wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) na Wakala wa Dhamana ya Uwekezaji wa Wahusika Anuwai (MIGA), matawi ya kibinafsi ya Benki ya Dunia. CAO inaripoti moja kwa moja kwa rais wa Benki ya Dunia, na wajibu wake ni kusaidia kutatua malalamishi kutoka kwa waathirika wa miradi iliyodhaminiwa na IFC/MIGA kwa njia ya haki, isiyo na upendeleo na ya kutoa maoni yanayosaidia, ili kuimarisha matokeo ya kijamii na ya kimazingira ya miradi hiyo.

Kupata maelezo zaidi, zuru www.cao-ombudsman.org.

**YALIYOMO**

**ORODHA YA AKRONIMU** ... iv
**1. MAELEZO YA JUMLA** ... 1
**2. USULI** ... 1
**2.1 Mradi** ... 1
**2.2 Malalamishi** ... 1
**3. MUHTASARI WA TATHMINI** ... 2
**3.1 Methodolojia** ... 2
**3.2 Muhtasari wa maoni** ... 2
**4. HATUA ZINAZOFUATWA** ... 15
**KIAMBATISHO A. Utaratibu unaofuatwa na CAO kushughulikia Malalamishi** ... 16

**ORODHA YA AKRONIMU**

| | |
|---|---|
| APBET | Njia Mbadala ya Kutoa Elimu na Mafunzo ya Msingi |
| CAO | Afisi ya Compliance Advisor Ombudsman |
| IFC | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| Bridge | Shule za Bridge International Academies |
| CDE | Mratibu wa Elimu wa Kaunti |
| EACHRights | East Africa Centre for Human Rights (Kituo cha Haki za Kibinadamu Afrika ya Mashariki) |
| KCPE | Cheti cha Elimu ya Shule ya Msingi ya Kenya |
| KICD | Taasisi ya Kukuza Mitaala ya Kenya |
| MoEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| TSC | Tume ya Kuajiri Walimu |

## 1. MAELEZO YA JUMLA

Mnamo Aprili 2018, CAO ilipokea malalamishi kutoka kwa East Africa Centre for Human Rights (EACHRights), Shirika lisilo la serikali (NGO) nchini Kenya, lililotoa malalamishi hayo kwa niaba ya wazazi na walimu kumi (10) wa sasa na wa awali, ambao ni ("Walalamishi"), kuhusiana na uwekezaji wa IFC kwa shule za Bridge International Academies ("Bridge" au "Kampuni") nchini Kenya. Walalamishi wanaibua suala la iwapo Kampuni inatimiza matakwa ya sheria za kimaitaifa na za taifa la Kenya pamoja na Viwango vya Utendakazi vya IFC. CAO ilitambua malalamishi hayo yanakubalika mwezi wa Mei 2018. Wakati wa tathmini iliyofanywa na CAO, Kampuni ilionyesha utayari wao kushiriki katika mchakato wa utatuzi wa mzozo, ilhali Walalamishi walipendelea kitengo cha CAO cha Ridhaa kishughulikie malalamishi yao. Kwa kuwa hawakuafikiana kuhusu njia muafaka zingetumika kutatua mzozo, ambazo ni za hiari, malalamishi yatapelekwa kwa kitengo cha Ridhaa cha CAO kutathmini utendakazi wa IFC kwa kuzingatia Maelekezo ya Operesheni ya CAO.

## 2. USULI

### 2.1 Mradi

Kwa mujibu wa IFC, Bridge ni mkusanyiko wa shule nyingi uliopiku zote barani Afrika zinazolipisha karo ya chini na kufikia Desemba 2018, Kampuni hiyo iliendelesha shule 297 zilizolipiwa karo na wazazi nchini Kenya. Kwa mujibu wa IFC, tangu mwaka wa 2009, Bridge imetoa mafunzo kwa walimu/viongozi wa shule 25,474, iliajiri walimu/viongozi wa shule 16,416 na kuwaelimisha wanafunzi 419,276 katika shule zake nchini Kenya. Mtandao wa shule hizo unapatikana kote nchini Kenya; mjini, vitongojini na sehemu za mashambani na zina nia ya kutoa elimu ya kiwango cha juu kwa watoto kutoka familia zinazopata chini ya dola mbili za Marekani kwa kila mtu kwa siku. Kulingana na taarifa walizonazo IFC, shule hizo zimejengwa na Bridge kwenye maeneo yasiyostawishwa yenye idadi ya watu wengi wenye kipato cha chini katika jamii ambako watoto hubidi kutembea mita zisizozidi 500 kufika shuleni. Kwa kuongezea, shule hizo zina njia zinazopitika kwa urahisi na zinaweza kufikiwa kupitia usafiri wa magari ya umma au ya kibinafsi[1]. Kufikia Februari 2019 uwekezaji wa IFC kwenye shule za Bridge ulifikia dola milioni 13.5 za Marekani kwa jumla kwa njia ya hisa zisizo na riba ya kudumu (ikiwa ni pamoja na haki miliki ya nyongeza ya hisa za mtaji), na pamoja na fedha kutoka kwa wawekezaji wengine, imewezesha kuweko kwa ongezeko la shule za Bridge nchini Kenya na kutanuka kwa kufunguliwa nyingine kwenye nchi tatu nyinginezo.

### 2.2 Malalamishi

Mnamo Aprili 2018, CAO ilipokea malalamishi kuhusu shule za Bridge kutoka kwa EACHRights yaliyotolewa kwa niaba ya watu 10 waliojitambulisha kama wazazi waliopo na wa awali, na walimu waliopo na wa awali wa Bridge ("Walalamishi"). Katika malalamishi, wanaibua suala la iwapo Kampuni inaridhia sheria za kimataifa na za kitaifa za Kenya, pamoja na Viwango vya Utendakazi vya 1, 2, na 4 vya IFC kuhusu hatari kwa mazingira na jamii, ajira na mazingira ya kufanyia kazi, na afya na usalama wa wanajamii. Malalamishi pia yalihusu ubaguzi kiuchumi, kutohusisha wazazi kwenye maamuzi na kutokuwa na uwazi hasa katika

[1] [1] Source: https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/32171

kuendesha masuala ya usimamizi wa shule kwa ujumla. Walalamishi wameomba kwamba utambulisho wao uhifadhiwe siri.

## 3. MUHTASARI WA TATHMINI

### 3.1 Methodolojia

Nia ya tathmini iliyofanywa na CAO ni kuweka bayana masuala yanayoibuliwa na Walalamishi, kukusanya taarifa kuhusu maoni ya washikadau mbalimbali na kubainisha iwapo Walalamishi na Wadhamini wa Mradi wa IFC wangependa kufuatilia utaratibu wa kutatua mzozo chini ya usaidizi wa CAO, au iwapo malamishi yapelekwe kwa kitengo cha Ridhaa cha CAO kuchunguza iwapo kanuni za utendakazi za IFC zilifuatwa, (tazama Kiambatisho A kuona hatua ambazo CAO hutumia kutatua mzozo). Kufikia hapa, CAO haitoi uamuzi iwapo malalamishi yanatambuliwa au la.

Hapa, tathmini ya malalamishi iliyofanywa na CAO ilihusisha:

- uhakiki wa nyaraka husika za mradi huu;
- mawasiliano ya simu, mapitio ya nyaraka zinazohusu mradi huu, na mikutano ya ana kwa ana na Walalamishi na NGO inayowaunga mkono;
- mawasiliano ya simu, mapitio ya nyaraka, na mkutano wa ana kwa ana na Bridge;
- mawasiliano ya simu na mkutano wa ana kwa ana na kikosi cha IFC kinachohusika na mradi;
- mikutano ya ana kwa ana na washikadau wengine waliopendekezwa na Walalamishi na Bridge; pamoja na
- ziara ya shule sita za Bridge zilizoko Nairobi, Homa Bay, Kisumu, na Mombasa.

Makala haya yanatoa muhtasari wa maoni yaliyosikilizwa na kikosi cha CAO kutoka kwa wahusika na yanafafanua hatua zitakazofuatwa kwa kuzingatia uamuzi uliochukuliwa na Walalamishi na Bridge.

### 3.2 Muhtasari wa Maoni

#### *3.2.1 Upande wa Walalamishi*

Wakati wa kutathmini, CAO ilikusanya taarifa zinazohusiana na malalamishi, zinazoweza kuwekwa katika makundi matatu:

1. Masuala ya udhibiti wa sheria
2. Masuala yanayohusiana na hali za ajira za walimu
3. Masuala yanayohusiana na mazingira ya shule

##### i. Masuala ya Udhibiti wa sheria

<u>*Kutosajiliwa kwa shule*</u>

Walalamishi walisema kuwa Bridge ilifungua shule yao ya kwanza Mukuru Kwa Njenga, eneo la vitongoji duni mjini Nairobi, Kenya, mwaka wa 2009. Idadi ya shule zinazoendeshwa na Bridge zimeongezeka baada ya hapo na kufikia mamia ya shule nchini kote. Walalamishi walisema kuwa kufikia sasa, nyingi ya shule za Bridge hazijasajiliwa kama inavyotakiwa na Sheria ya Elimu ya Msingi ya mwaka wa 2013, na kwa hivyo, hawana kibali cha kuendesha shughuli. Walalamishi walieleza kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST)

itakayorejelewa kama “Wizara ya Elimu”), iligundua kuwa shule za Bridge hazikuwa zimesajiliwa kufikia Oktoba 2014, wakati Bridge ilipotaka kusajili wanafunzi mwaka wa 2015 ili kufanya mtihani wa kitaifa wa kuhitimu masomo ya shule ya msingi (KCPE). Waliendelea kwa kusema kuwa hapo, Wizara ya Elimu iliwaandikia Waratibu wote wa Elimu wa Kaunti (CDEs), wanaowakilisha Wizara kwenye ngazi ya kaunti, ikisema kuwa kila shule sharti isajiliwe kivyake. Wakati huo, Bridge ilikuwa tayari imeasisi shule takribani 250. CDE's walishauriwa na Wizara kukagua, ikiwa ni pamoja na mambo mengine, kuwa kila shule:

- ilisajiliwa kivyake kama shule ya kibinafsi kwa kuzingatia vipengele vya Sheria na Kanuni za Elimu ya Msingi za mwaka wa 2015, badala ya kupewa leseni moja;
- zilifuata Mtaala wa Kitaifa wa Kenya wa 8-4-4 (miaka minane ya masomo ya shule ya msingi, miaka minne ya masomo ya shule ya upili na miaka minne ya masomo ya chuo kikuu), na ilifuata ratiba ya mpangilio wa vipindi; na
- zina walimu waliohitimu na kusajiliwa na Tume ya Kuwaajiri Walimu.

Walalamishi pia walieleza kuwa shule za Bridge zilianzishwa kwa sababu serikali ya Kenya haikuwa na mpangilio mzuri wa kutoa elimu katika vitongoji duni. Kutokana na hali hiyo, jamii zilianza kujipanga na kuanzisha shule zisizokuwa rasmi ambazo hazikuwa zinadhibitiwa na serikali. Kwa mujibu wa Walalamishi, katika mwaka wa 2012, serikali ilianza kukuza mwongozo wa kusajili shule zinazotumia Njia Mbadala ya Kutoa Elimu na Mafunzo ya Msingi (APBET) kwa nia ya kuhudumia jamii zinazopatikana katika vitongoji duni katika miji ya Nairobi, Mombasa, na Kisumu, pamoja na maeneo kame kiasi na maeneo kame kabisa. Mwongozo wa APBET ulizinduliwa mwezi wa Machi 2016. Walalamishi walieleza kuwa Bridge, ambao kwa wakati huo walikuwa wameelekezwa kusajili shule zake kama shule za kibinafsi, walijaribu kubadili hali ya usajili, wakiwa na matumaini kuwa shule zao zingechukuliwa kama taasisi za APBET. Hii ni kwa sababu vigezo vya usajili wa shule za APBET vililegezwa kidogo ili kuwezesha mtandao wa shule zisizokuwa rasmi kwa muda mrefu kurasimishwa. Walalamishi walisema kuwa, Machi 2016, Wizara ya Elimu ilitathmini shule 61 za Bridge na kufikia uamuzi kuwa hazikufuzu kusajiliwa kama taasisi za APBET, na kuwa shule za Bridge zilipaswa kusajiliwa kama taasisi za kibinafsi. Wizara, kwa hivyo, iliipa Bridge siku 90 kutimiza matakwa ya mwongozo uliowekwa, la sivyo, shule hizo zingefungwa kufikia Novemba mwaka wa 2016. Walalamishi walieleza kuwa katika mwezi wa Juni 2017, Wizara ililalamikia kwa mara nyingine hali ya Bridge ya kutosajiliwa na kusisitiza kuwa shule za Bridge hazina sifa za APBET.

Walalamishi waliongeza ya kuwa, mwaka wa 2014, Bodi ya Elimu ya Kaunti ya Busia (CEB) iliamua kufunga shule 10 kati ya 12 za Bridge kwa kwenda kinyume cha sheria za Kenya na kuwa Bridge ilienda kortini kupinga hatua hii. Kwa mujibu wa Walalamishi, mahakama ilikubaliana na uamuzi wa CEB na kuiamuru kaunti ya Busia kuwatafutia wanafunzi shule mbadala kabla ya kufungwa kwa shule hizo. Shule hizo bado zimefunguliwa bila ya kusajiliwa kwa sababu Bridge ilirudi mahakamani kupinga uamuzi wa korti, na kukubaliwa ombi lao kwa amri ya kisheria la kuzuia kufungwa kwa shule hizo. Hata hivyo, kulingana na Walalamishi, ukaguzi mpya uliamrishwa kufanywa na Wizara ya Elimu mwezi wa Agosti mwaka wa 2018, kuthibitisha iwapo shule hizo zinafuata viwango vilivyowekwa. Ukaguzi huu unapaswa kufanywa mwanzoni mwa mwaka wa 2019.

*<u>Kutumia walimu wasiohitimu</u>*

Walalamishi walidai ya kuwa mwanzoni, Brigde ilikuwa na mtindo wa kutumia walimu wasiohitimu, walio na cheti cha Mtihani wa Shule ya Upili (KCSE), kwa sababu walimu hao walipewa kompyuta ya walimu yenye andao la somo lililotungwa kwa kila somo. Wanashikilia

kuwa haya ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Elimu ya Msingi ya 2013, inayowataka walimu wote wawe wamehitimu na kusajiliwa na Tume ya Kuajiri Walimu.

Walalamishi walielezea kuwa, mnamo Aprili 2017, Bridge ilisema ya kuwa Mwongozo wa APBET ulitaka shule hizo kuwa na asilimia 30 tu ya walimu waliohitimu na kusajliliwa na Tume ya Kuajiri Walimu, kufikia miaka mitatu baada ya kuajiriwa na taasisi. Hata hivyo, mnamo Juni 2017, Wizara ya Elimu ilidokezea Bridge, hasa kwa kuzingatia Mwongozo wa APBET, kuwa:

- wakati wa kusajili taasisi, asilimia isiyopungua 30 ya walimu kwenye taasisi wanapaswa kuwa na cheti mwafaka cha walimu kutoka katika taasisi ya kuwafundisha walimu inayotambulika na wawe wamesajiliwa na Tume ya Kuajiri Walimu (TSC), kabla ya kuajiriwa;
- asilimia 70 waliosalia sharti wawe wanaendelea na mafunzo wakati wanafanya kazi; na
- wasimamizi wa taasisi wataendelea kuhakikisha ya kuwa walimu wao wote wamesajiliwa na TSC ifikiapo miaka mitatu baada ya taasisi kusajiliwa, ikimaanisha kuwa kufikia mwaka wa tatu tangu kuanzishwa, asilimia 100 ya walimu sharti wawe wamefuzu na kusajiliwa na TSC.

Walalamishi walidai ya kuwa kufikia tarehe waliotoa malalamishi, Bridge ilikuwa bado inatumia walimu wasiohitimu wala kusajiliwa hata baada ya kuwepo kwa zaidi ya miaka mitatu na kuwa, juhudi zilizofanywa na Bridge kuongeza idadi ya walimu waliohitimu imetokana na hamasisho kutoka kwa makundi ya kijamii.

*<u>Kutumia Mtaala usiokuwa wa Kenya</u>*

Walalamishi walieleza ya kuwa shule nchini Kenya zinaweza kutumia mtaala wa kimataifa au wa kitaifa. Bila kuzingatia ni mtaala upi unaotumiwa, kila shule inatarajiwa kupeleka mtaala wake kwa Taasisi ya Kukuza Mitaala ya Kenya (KICD) ili kutathminiwa na kuidhinishwa.

Walalamishi walieleza ya kuwa Bridge haitumii mtaala wa kitaifa, kinyume na wanavyodai, na haijatimiza matakwa ya KICD. Walalamishi walieleza kuwa Bridge ilifanya mikutano na Wizara ya Elimu mwaka wa 2014, ikiomba kutathminiwa vitabu inavyotumia kufunzia madarasa ya 1 hadi 8. Wizara ya Elimu iliwatuma kwenda KICD. Baadaye, Bridge ilipopeleka vifaa vyao vya kufundishia kutathminiwa, KICD haikuviidhinisha. Walalamishi wanaamini kuwa Bridge haitumii hata mojawapo ya vitabu sita vilivyoidhinishwa na KICD (kwa kila somo) na vitabu vyao vya ziada haviambatani na mtaala wa Kenya kwa sababu havijaidhinishwa na KICD.

Walalamishi walisema kuwa Bridge iliomba ipewe mafunzo kutoka kwa KICD kuwawezesha kufafanua mtaala wa Kenya na kukuza vitabu vya ziada vinavyoafikiana na mtaala. Walipokea mafunzo kutoka KICD. Hata hivyo, kwa mujibu wa Walalamishi, baada ya mafunzo ya mwaka wa 2015, Bridge iliwasilisha tena vitabu vyao kutathminiwa upya. Vitabu hivyo vilitathminiwa na jopo la wataalamu sita na havikuidhinishwa. Baadaye, ripoti kuhusu suala hili ilipelekwa kwa Wizara ya Elimu na KICD. Kwa mujibu wa Walalamishi, tangu mwaka wa 2015 Bridge haijatuma vitabu vyao kutathminiwa tena.

### ii. Masuala yanayohusiana na hali za ajira za walimu

*<u>Muda mwingi wa kazi kwa mshahara duni</u>*

Walalamishi walisema kuwa walimu wa Bridge hufanya kazi muda mwingi, hali iliyo kinyume cha katiba ya Kenya ya 2010 na Sheria za Elimu ya Msingi za 2015. Walisema kuwa walimu wanatarajiwa kufanya kazi masaa kumi kwa siku kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na masaa sita siku za Jumamosi, na kuwa huu ni muda mrefu kuliko inavyotakikana kwa mujibu wa sheria za kitaifa. Walalamishi walidai kuwa Bridge hailipi fidia kwa muda wa ziada na kuwa walimu hawana muda wowote wa mapumziko. Walalamishi walisema kuwa wakati wa kipindi cha mapumziko cha muda wa dakika 15 ili kunywa chai, na kipindi cha mapumziko cha dakika 40 cha chakula cha mchana ambazo walimu wanapaswa kupewa, wanatarajiwa kuwaangalia watoto wanapocheza. Kwa kuongezea, hakuna vitu kama vile chumba cha walimu ili kutumiwa wakati wa mapumziko au wa kula katika shule zote za Bridge nchini Kenya.

Walalamishi wanaamini kuwa mshahara wa walimu ni wa kiwango cha chini kuliko inavyodokezwa na mwongozo wa kitaifa. Walisema kuwa kufikia 2017 walimu walidaiwa kulipwa kati ya $88 na $150 kwa mwezi, ambapo aghalabu ni kima cha chini sana kuliko mshahara unaopendekezwa katika Agizo la Kanuni za Mshahara. Walalamishi walieleza kuwa, ijapokuwa walimu hupokea mshahara wao kwa wakati unaofaa tofauti na shule zilizo kwenye kundi moja na Bridge, na kwa kuwa mshahara ni duni ukilinganishwa na shule nyinginezo, walimu mara kwa mara hutafuta nafasi za kupata kazi zingine zinazolipa vizuri.

*Nidhamu*

Walalamishi walidai ya kuwa waajiriwa hufanyiwa mambo yasiyofaa na hata kuachishwa kazi kwa njia isiyofaa. Walieleza kuwa Bridge huwaachisha walimu kazi bila kuwaeleza makosa yao au kuwapa fursa ya kujieleza kuhusiana na makosa wanayodaiwa kuyafanya. Walisema kuwa wafanyikazi pia wameachishwa kazi kwa kutaka kujua kwa nini kampuni ilikuwa na sera mbovu. Walalamishi walisema kuna wakati ambapo mwajiriwa aliyefutwa kazi alipelekwa mahakamani na Bridge ili azuiliwe kufanya kazi kuhusiana na kipengelee kinachosema ya kuwa mwajiriwa huyo azuiliwe kuanzisha shule wala kuajiriwa shuleni au kwenye taasisi yoyote inatoa huduma za moja kwa moja au zisizokuwa za moja kwa moja zinazoingiliana na zile zinazotolewa na Bridge kwa muda wa miaka miwili. Koti ilitupilia mbali kesi hiyo. Walalamishi pia walidai ya kwamba baada ya kuachishwa kazi, wafanyikazi hawakulipwa mshahara wa mwisho kabla ya kufutwa.

*Matumizi ya kompyuta za walimu*

Walalamishi walieleza kuwa Bridge huhitaji walimu kutumia kompyuta za walimu kufundisha wanafunzi na kuwa kila asubuhi, walimu hupata makala ya kufundishia ya siku hiyo kwenye kompyuta za walimu na wanatakiwa kuyafuata makala yaliyomo kikamilifu bila kuongezea wala kupunguza. Walalamishi walijulisha CAO ya kuwa, ijapokuwa kuna walimu ambao hufurahia hali ya kutojiandalia makala yao ya kufundishia, ukosefu wa uwezo wa kutotumia makala hayo huangamiza ubunifu miongoni mwa walimu. Pia haitoi fursa kwa walimu kutoa muda zaidi kwa wanafunzi wanaosalia nyuma ya wenzao. Walalamishi walieleza kuwa kompyuta za walimu zina saa zilizodhibitiwa kwenye komputa zinazowaonyesha walimu ikiwa wakati wa kusonga kwenye sehemu nyingine umefika. Iwapo mwalimu atakosa kumaliza somo la siku, itachukuliwa kuwa utendakazi wake ni duni na hata anaweza kufutwa kazi. Zaidi ya hayo, wanadai kuwa walimu hawawezi kurudi kwa vipindi vya somo vilivyopita kwa sababu makala ya vipindi hivyo hujifuta kutoka kwenye kompyuta za walimu baada ya kutumiwa.

*Kutafuta Wateja*

Walalamishi walieleza kuwa walimu walitakiwa kutafuta wateja wakati wa likizo ya Aprili, Agosti, na Desemba. Walisema kuwa kila mwalimu anapewa idadi ya wanafunzi wapya wanaopaswa kusajiliwa shuleni. Kwa mujibu wa Walalamishi, idadi hiyo inaweza kuwa isiyowezekana kufikiwa, na mwalimu anapokosa kufikisha idadi aliyopewa, anachukuliwa

hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kupunguzwa mshahara wao kwa kiwango fulani. Walalamishi waliongezea kuwa idadi kubwa ambayo kila mwalimu hupewa ilisababisha matatizo kati ya walimu na wanajamii. Hii ni kwa sababu walimu huishi kwa jamii ambamo wanatafuta wateja. Baada ya kwenda mara kadhaa kwa wanajamii, wao huanza kuonekana kama kero.

Walalamishi walisema kuwa Bridge iliwahimiza kueleza wazazi watarajiwa kuwa wanao wangepokea ufadhili iwapo wangejiunga na Bridge. Walieleza kuwa mara nyingi, ahadi hii ilikuwa ya uongo ili kuwavutia wazazi shuleni humo. Ijapokuwa baadhi ya wanafunzi hupata ufadhili wanaostahili kupata, Walamishi walieleza ya kuwa wanafunzi wengi wanaoahidiwa ufadhili hawaupati. Hali hii husababishia wazazi wanaosajili watoto wao katika shule za Bridge matatizo wanao wanapokosa ufadhili. Walieleza kuwa, baada ya ufadhili kukosekana, wazazi hulazimika kulipia wanao karo ya shule za Bridge wanayoiona kuwa ghali. Pia, walieleza kuwa kuna wakati mwingine, hata kama mtoto amepokea ufadhili, ufadhili husitishwa, na hii hulazimu wazazi wao kutafuta pesa ya kulipa karo. Waliezea tena kuwa pale ambapo wazazi wanashindwa kulipa karo, mwanafunzi hufukuzwa shuleni. Walalamishi walisema kuwa wakati mwingine haya hutokea mwaka unapoelekea kwisha na hali hii hupelekea wazazi kupata changamoto ya kutafutia wanao shule nyingine. Walidai hali hii hupeleka wanafunzi kutomalizia mwaka shuleni na hivyo basi kulazimika kurudia darasa. Walalamishi walidai pia kuwa ufadhili ulitolewa kwa njia ya ubaguzi kiasi kwamba kuna makundi yaliyopendelewa kuliko mengine.

*Hali nyinginezo za kufanyia kazi*
Walalamishi walidai ya kuwa walimu walifanya kazi kwa hofu na hata kudhalalishwa, na kuwa, kila mara, wanahofia kupoteza kazi zao, au mshahara wao kupunguzwa kwa maswala kama vile kukosa kupifikisha idadi ya wanafunzi uliyopewa wakati wa kutafuta wateja, kuchelewa kufika shuleni au kuruhusu wanafunzi walio na deni kuhudhuria vipindi.

### iii. Masuala yanayohusiana na mazingira ya shule

*Karo*
Kulingana na Walalamishi, karo ya shule ambayo ni kati ya $6.40 - $10.57 kwa mwezi kugharamia ada ya mafundisho, hufanya shule hizo kutohudumia watu ambao kampuni hiyo hudai hulenga, yaani watu walio na ujira duni wanaoishi kwa kutumia chini ya $2 kwa siku. Zaidi ya hayo, wanasema, ikilinganishwa na shule zingine za aina hiyo kwa maeneo hayo, shule za Bridge hazina mpangilio wa jinsi ya kupata chakula na kwa hivyo, wazazi wanalazimika kulipa zaidi ili kuhakikisha wana wao wanapata chakula cha mchana. Walalamishi walieleza pia kuwa karo ya shule, ada ya usajili (shilingi 700), bei ya sare ya shule, hela za kulipia mtihani ikijumuishwa pamoja ni ghali kuliko inavyotangazwa na huongezeka kila mwaka bila kuwajulisha walimu na wazazi kwanza. Walalamishi pia walirejelea utafiti uliofanywa mwaka wa 2016 na Education International na Chama cha Kitaifa cha Walimu. Utafiti huu ulionyesha asilimia 58 ya wanafunzi wa Bridge walioshiriki kwenye utafiti waliwahi kosa kwenda shuleni kwa kukosa kulipa karo na kuwa, kati ya asilimia 69 hadi 83 ya wazazi walioshiriki kwenye utafiti huu walidokeza kuwa walikuwa na changamoto ya kulipa karo na vitu vingine ikiwa ni pamoja na matibabu, chakula na kodi ya nyumba. Walalamishi pia walidokeza kuwa, katika hali nyinginezo, wanafunzi wamefukuzwa kutoka shuleni hata kama deni lao lilikuwa shilingi hamsini tu, hata wakiwa karibu kufanya mtihani wa kitaifa. Walieleza kuwa sera ya kufukuza wanafunzi darasani kwa kutolipa karo hufanywa tu na walimu, wanaotarajiwa kufanya hivyo kwa kutoruhusu watoto ambao hawajamaliza kulipa karo kushiriki vipindi. Walalamishi walieleza pia kuwa walimu wangeadhibiwa iwapo wangeruhusu

wanafunzi ambao hawajalipa karo kuhudhuria vipindi. Hii hufanywa kwa kukata pesa kutoka kwa mshahara wao.

*Hali na Mahali Shule zinapatikana*
Walalamishi walijulisha CAO kuwa shule nyingi za Bridge zilikuwa katika hali ya kukatisha tamaa na hazikuwa na vifaa vyovyote vinavyoweza kutumiwa na watoto walemavu. Wanadai kuwa shule nyingine hazina nafasi ya kutosha ya kuchezea na iwapo kuna viwanja vya kuchezea, hufurika wakati wa mvua, hali inayosababisha matope mengi mno.

Walalamishi walionyesha kuwa hawakuridhishwa na hali ya vyoo katika baadhi ya shule ambavyo vina hali ya kukatisha tamaa. Walielezea kuwa katika Kaunti ya Nyeri, kesi nyingi zilipelekwa mahakamani dhidi ya Bridge ili kujaribu kufunga shule hizo kwa sababu, mbali na mambo mengine, hali ya vyoo haikuridhisha kabisa, na ya kuwa, hawakuzingatia mgao wa choo kimoja kwa wanafunzi 25 jinsi inavyotakiwa kisheria.

Kulingana na Walalamishi, shule zingine zimejengwa karibu na kichinjio au maduka ya pombe na shule zingine hazikuwa na kuta au vizingiti vya usalama, hali ambayo ilisababisha ukosefu wa usalama kwa shule na kwa wanafunzi. Walieleza kuwa jikoni zilikuwa kwa hali mbaya, na shule zingine zinapatikana karibu na mashimo makubwa ya taka au kando ya mabomba ya kupitisha uchafu. Walalamishi pia walisisitiza kuwa, kabla ya ziara ya Kutathmini ilyofanywa na CAO, Bridge ilisafisha shule ili zionekane kuwa bora.

Walalamishi walieleza kuwa shule za Bridge hazikuwa na magodoro ya kulalia watoto wa chekechea wakati wa kulala ili kupumzika unapofika na ya kuwa, watoto hulala kwenye dawati zao. Walisema kuwa, shule hizo hazina vifaa vya kudhibiti joto madarasani kwa sababu shule nyingi hutengenezwa kwa mabati. Wakati wa baridi madarasa huwa baridi na wakati wa joto madarasa huwa na joto. Walalamishi wanaamini kuwa mazingira haya siyo mazuri ya kusomea. Kwa kuongezea, Walalamishi walisema ijapokuwa Bridge inasema inatoa elimu ya kiwango cha juu kwa kuwa na madarasa yalio na wanafunzi wachache, kuna madarasa yalio na wanafunzi wengi wanaoweza kufika 63. Hii ni changamoto hasa wakati wa joto. Walalamishi walidokeza pia kuwa madarasa hayana stima hali inayowafanya wanafunzi kusoma kwa ugumu iwapo kuna giza nje au wakati wa mvua.

### *3.2.2 Upande wa Kampuni*

**i. Masuala ya Udhibiti wa sheria**

*Kutosajiliwa kwa shule*
Bridge ilieleza kuwa katika mwaka wa 2009, walipofungua shule yao ya kwanza, walipokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu ikiwajulisha kuwa hapakuwepo na sera ya kusajili shule zisizokuwa rasmi. Wizara ilijulisha Bridge ya kuwa shule zake zingesajiliwa pindi tu Sera ya Shule Zisizokuwa Rasmi itakapokuwa tayari. Hata hivyo, kwenye hiyo barua, Wizara ilitambua kuwa, jinsi ilivyo, Bridge ilitimiza vigezo vyote vya kuiwezesha kusajiliwa kama shule zisizo rasmi. Bridge pia ilieleza ya kuwa iliendelea kuwasiliana na Wizara hiyo tangu mwaka wa 2009 na kuwa walihusishwa katika mikutano yote ya kitaifa ya washikadau ikuhusu mijadala juu ya shule zisizokuwa rasmi. Pia, walihusishwa katika kuandika mswada wa mwongozo wa Njia Mbadala za Kutoa Elimu na Mafunzo ya Msingi (APBET) utakaowezesha kusajiliwa kwa shule mbadala au zisizokuwa rasmi. Mwongozo huu ulipaswa kutolewa kila mwaka tangu mwaka wa 2009, lakini hali haikuwa hivyo hadi Machi 2016. Bridge ilieleza ya

kwamba, kati ya mwaka wa 2013 na 2016, kulikuwa na madadiliko katika serikali ya kitaifa hasa kwenye sekta ya elimu, yakiwemo mabadiliko ya kikanuni, hali iliyopelekea kupitishwa kwa Sheria ya Elimu ya Msingi ya mwaka wa 2013 na sheria nyingine sita zinazohusiana na elimu. Shule za umma na za kibinafsi nchini Kenya ziliathiriwa na mabadiliko hayo ya kisheria na zilipaswa kufuata kanuni mpya.

Bridge ilipinga madai kuwa ilienda kinyume cha sheria na kuwa Wizara ya Elimu haikufahamu uwepo wao kabla ya Octoba 2014. Bridge iliongezea kuwa, mnamo mwaka wa 2013, kwa mujibu wa Sheria za Elimu zilizokuwepo wakati huo, ambapo Baraza la Mitihani ya Kitaifa ya Kenya (KNEC) lilitoa idhini ya awali kwa shule zote za Bridge (zilizokuwa 134) zisajiliwe kama vituo vya kufanyia mtihani vikingojea kuidhinishwa na Wizara. Hata hivyo, kutokana na kanuni za mwaka wa 2012 za mtihani wa Cheti cha Elimu ya Shule ya Msingi (KCPE), Wizara ilifuta idhini ya hapo awali iliyokuwa ikisema kuwa chini ya kanuni za mwaka wa 2012, shule zote zisizo rasmi zinapaswa kusajiliwa kabla ya kutumiwa kama vituo vya kufanyia mtihani. Licha ya hayo, Bridge ilifanikiwa kusajili kwa muda shule 63 kati ya shule zake kama shule za kibinafsi na Wizara ya Elimu. Baadaye shule hizo 63 zilisajiliwa na kuruhusiwa kutumika kama vituo vya mtihani na kuwasilisha watahiniwa wake wa 2015.

Bridge pia ilieleza kuwa iliendelea kuwa na mafungamano na Wizara ya Elimu katika muda huo wote. Wakati ambapo Wizara ilidai Mwongozo wa APBET uliotolewa mwaka wa 2016 kutofuatwa, Kamati ya Wizara ikiongozwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kuhakikisha Viwango na Ubora wa Elimu ilibuniwa ili kufanya kazi pamoja na Bridge kupanga mkakati wa hatua za kutimiza matakwa ya viwango. Bridge ilieleza kuwa ilikuwa ikituma ripoti kila mwezi kwa kamati husika juu ya hali yao ya kutimiza matakwa ya viwango vya Mwongozo wa APBET. Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki cha kutoa ripoti, mwezi wa Agosti 2018, Wizara ya Elimu ilithibitisha kuwa Bridge ilikuwa ikiwasilisha ripoti hizo mara kwa mara. Wizara ikaelekeza timu ya Kuhakikisha Ubora kutathmini tena kiwango cha kutimiza matakwa ya viwango cha shule zote za Bridge, kwa nia ya kuzisajili kama shule za kibinafsi zisizokuwa rasmi na siyo kama shule za kibinafsi, iwapo watatimiza viwango vya chini vinavyohitajika. Bridge ilielezea CAO kuwa hatua ya ukaguzi ilikuwa imeanza, na kufikia Oktoba 2018, shule 189 zilikuwa zimepokea ripoti nzuri ya Ukaguzi wa Afya ya Umma, na shule 50 zilikuwa zimepokea ripoti nzuri ya Uhakikisho wa Ubora. Bridge inasubiri ripoti zilizosalia na inapiga hatua ya kufuatilia na kusajili shule zilizotathminiwa.

Kuhusu kesi za kortini kwenye kaunti ya Busia, Bridge ilieleza kuwa wakati Mwongozo wa APBET ulipochapishwa mwaka wa 2016, Wizara ya Elimu na Bodi za Kaunti za Elimu (CEB) zilitofautiana jinsi ya kutekeleza mwongozo huo, hasa juu ya matakwa ya usajili. Kwa sababu hiyo, shule 10 kati ya 12 za Bridge katika kaunti ya Busia zilikabiliwa na kesi mahakamani, na CEB ilikataa ombi la kusajili shule hizo kama za APBET na kuamuru zifungwe. Walieleza kuwa walienda mahakamani kupinga uamuzi wa sheria wa kufunga shule hizo. Mahakama ilishikilia amri ya CEB ya kufunga shule hizo. Kwa hivyo Bridge ilitoa wito kwa CEB kusajili shule zao kama za kibinafsi. Hata hivyo, CEB ilitupilia mbali ombi hilo na baada ya kujaribu mara kadhaa na kushindwa kupata suluhu kutoka kwa serikali ya kaunti, ikiwa ni pamoja na kuendea Tume ya Utawala wa Haki ili kuomba sheria hiyo iangaliwe upya, Bridge haikupata majibu na ikabidi warudi kortini.

Bridge ilieleza ya kuwa wakati huo, Mahakama ilitoa uamuzi kuiruhusu kuendelea kufanya kazi ikisubiri Uamuzi Mpya wa Jaji na kuruhusu Bridge kuandikia CEB barua wakiomba kusajiliwa kama shule ya kibnafsi. Ombi hilo lilitolewa na linasubiri kufanyiwa uamuzi. Hata hivyo, shule zote za Bridge bado zinaendelea kufanya kazi. Bridge pia ilieleza CAO kuwa Gavana na Naibu

wa Gavana katika Kaunti ya Busia wanaunga mkono kuwepo kwa shule za Bridge katika kaunti. Bridge inaendelea kufanya kazi na CEB ili kuhakikisha ya kuwa shule zao zinasajiliwa.

*Kutumia walimu wasiohitimu*

Bridge ilidokeza kuwa shule zao zote zilitimiza matakwa ya walimu yanayopatikana katika Mwongozo wa APBET. Mwongozo unazitaka shule zisizo rasmi kuwa na idadi isiyopungua asilimia 30 ya walimu waliohitimu wakati wa kusajiliwa kwake, na waliosalia wakiendelea na masomo yao wanapofundisha. Bridge ilidokeza pia kuwa Tume ya Kuajiri Walimu nchini Kenya ilisema kuwa kulikuwa na upungufu mkubwa wa walimu katika shule za msingi na zile za sekondari. Bridge pia ilieleza kuwa katika maeneo kame kabisa na kame kiasi na hasa kwenye maeneo ya shidashida, inapitia changamoto zilezile zinazokabili shule zingine za kibinafsi na zile za umma wakati wa kuajiri na kuhifadhi walimu waliohitimu. Hii inatokana na changamoto ya ukosefu wa usalama unaotishia walimu kutovutiwa kufanya kazi huko. Hata kama hali hii inaendelea kuwa changamoto kwa sekta nzima ya elimu, Bridge ilieleza kuwa huwasaidia walimu wake wote kwenye maeneo yalio na shidashida ili kuhakikisha wanafanya kazi kwa kutumia mtaala wa kitaifa ili kupata matokeo yanayotarajiwa. Bridge ilieleza ilivyo sasa, imeajiri zaidi ya asilimia 30 ya walimu waliohitimu na kuhakikisha ya kwamba wale ambao hawajahitimu wanaendelea na masomo yao huku wakifundisha. Bridge iliongezea kuwa, kutoka Machi 2016, walipoanza kutoa ripoti kwa Wizara ya Elimu kama sehemu ya kutimiza matakwa ya viwango, kumekuwa na ongezeko la idadi ya walimu waliopata mafunzo yao kutoka kwa taasisi za serikali kwenye shule zake. Tangu mwaka wa 2009, Bridge ilisema kuwa imefunza walimu/viongozi wa shule 25,474 na kuwaajiri walimu/viongozi wa shule 16,416. Kulingana na Bridge wamepitisha uamuzi wa kisera wa kuajiri tu walimu waliohitimu wa kiwango cha P1 na wanawasaidia walimu wote ambao hawana kiwango au cheti hiki kujiandikisha kupata mafunzo huku wakifundisha.

Bridge pia ilidokeza kuwa hapo awali, serikali iliajiri walimu wasiohitimu. Hii ni kutokana na upungufu mkubwa wa walimu nchini Kenya. Bridge ilieleza kuwa, bila kuzingatia uzoefu wa walimu, wanapoajiriwa na Bridge, wanapokea maelekezo ya kina kabla ya kuanza kufundisha. Kwa kuongezea, walimu huendelea kupokea mafunzo ya mara kwa mara ili kuwakuza huku wakifanya kazi.

*Kutumia mtaala usiokuwa wa Kenya*

Bridge ilieleza kuwa, kinyume na wanavyodai Walalamishi, shule zao zote hutumia mtaala wa kitaifa wa 8-4-4, au ule mtaala mpya wa kitaifa uitwao CBC - Mtaala Unaozingatia Umilisi (2-6-3-3) katika madarasa ambayo tayari yameanzishwa. Bridge ilieleza ilikuwa imeanza kutumia mtaala mpya na walikuwa wakishiriki katika mafunzo ya walimu yaliyoandaliwa na serikali ya kaunti na kuchangia pakubwa katika mchakato wa kuleta mageuzi ya kimtaala nchini Kenya na kuwa walichaguliwa kushiriki katika majaribio na Serikali.

Bridge pia ilieleza ya kwamba walishirikiana na kuwasilisha vitabu vya wanafunzi na miongozo ya walimu kwa Taasisi ya Kukuza Mitaala ya Kenya (KICD) ili kutathminiwa iwapo vinaambatana na mtaala wa 8-4-4. Waliongezea ya kwamba si tu eti wanafuata mtaala wa kitaifa ulioidhinishwa wa 8-4-4, bali wanafunzi wa darasa la nane waliotahiniwa kwa mtihani wa kitaifa wa (KCPE) mwaka wa 2015 walipata alama ya wastani iliyokuwa juu kuliko ya kitaifa,

huku zaidi ya wanafunzi 50 wakipata nafasi katika shule za kitaifa. Bridge ilielezea CAO kuwa, mwaka wa 2016 shule zake ziliainishwa kama za kwanza kwenye wilaya nyingi zikiwemo Nyakach, Ugunja, Bondo, na Machakos. Katika mwaka wa 2017, zaidi ya wanafunzi 1,000 walipata alama zaidi ya ile alama ya wastani kwenye KCPE, na zaidi ya wanafunzi 100 walipata nafasi kuteuliwa katika shule za kitaifa za kifahari nchini Kenya. Wanafunzi wengine 3,400 walitarajiwa kufanya mtihani wao wa KCPE Novemba 2018. Bridge ilieleza kuwa, kwa miaka mitatu iliyopita, takribani watoto 10,000 walifanya mtihani wa KCPE na kuhitimu kutoka shule za Bridge. Hali haingekuwa hivi iwapo wangetumia mtaala mwingine usiotumiwa nchini.

**ii) Masuala yanayohusiana na hali za ajira za walimu**

*<u>Muda mwingi wa kazi kwa mshahara duni</u>*

Bridge ilieleza kuwa wametangazwa kuwa mojawapo ya waajiri kumi bora zaidi barani Afrika mwaka wa 2018. Walisema kuwa walilipa walimu wao wote zaidi ya kiwango cha chini cha mshahara na kuwa walimu wao wengi walilipwa asilimia 20 zaidi ya kiwango cha chini cha mshahara kilichokubalika, ikiwemo idadi kubwa ya walimu wao wakipokea asilimia 55 au zaidi ya mshahara wa chini. Kwa mujibu wa Bridge, wana mazoea ya kufanya utafiti mara kwa mara ili kulinganisha mshahara wao na wa shule zinginezo za kibinafsi katika jamii zinapopatikana shule zao na kila uchao wao huibuka kama shule inayolipa vizuri licha ya kulipisha karo kidogo.

Kuhusu muda wa kufanya kazi walimu, Bridge ilisema kuwa walifuata Sheria ya Taasisi za Ajira inayoruhusu wafanyikazi kufanya kazi kwa muda wa ziada (zaidi ya saa 52 kwa juma), maadamu watalipwa kiwango cha 1.5 kwa kazi ya ziada, na kuwa hawakufanya kazi zaidi ya saa 116 kwa muda wa majuma mawili yoyote. Bridge ilitetea kuwa wakati wa muda wa mapumziko, kama ilivyo katika shule nyingi, wanaweza kuomba baadhi ya walimu kuwafuatilia na kuwasimamia watoto wanapocheza.

Bridge ilidokeza pia kwamba, kutokana na mchoro sanifu wa shule, hawakutenga chumba kando cha kutumiwa na walimu. Hii ni kwa sababu walimu hupewa miongozo ya walimu na maazimio ya kazi kwenye kompyuta zao, hali inayopunguza muda wanaohitaji walimu kujiandaa kwa ajili ya vipindi na huongezea muda wa walimu kujumuika na wanafunzi, kinyume na mtindo utakaomfanya mwalimu kutumia muda mwingi kwenye chumba cha walimu wakiandaa masomo.

*<u>Nidhamu</u>*

Bridge ilieleza kuwa walimu wote walioachishwa kazi waliachishwa kwa kufuata Sheria za Ajira. Na iwapo mwajiriwa hakuridhishwa na sababu, jinsi, na/au utaratibu wa kufutwa kazi, Bridge ina mfumo wa ndani kwa ndani unaoweza kutumiwa na waajiriwa kutoa malalamishi yao. Kuongezea, Sheria za Ajira zinatoa njia ya kuomba kusikilizwa tena, ambayo ni pamoja na kuripoti kwa Afisi ya Ajira na kutoa malalamishi kwa Mahakama ya Ajira na Mahusiano Kazini kuhusu kuachishwa kazi kinyume na sheria kwa njia isiyofaa. Bridge ilieleza kuwa walimu hupoteza kazi kutokana na sababu, mfano utendakazi wao na makosa kazini. Katika hali zote zinginezo, wao walisema kuwa hulenga kuhifadhi na kukuza wafanyikazi wao.

Kuhusiana na vifungu vya kuzuia ushindani, Bridge ilielezea CAO kuwa mkataba wao wa ajira una vipengele vya kuzuia ushindani na kujihusisha na mambo yanayoihusu. Kwa mujibu wa Bridge, kuwepo kwa vipengele hivi kwenye mkataba wa ajira ni ishara kuwa waajiriwa hawajawekewa shinikizo "lisilokuwa la kawaida". Waliendelea kwa kueleza kuwa, mtu anayetaka kuajiriwa ana haki ya kukataa kazi iwapo kuna vipengele kwenye mkataba asivyokubaliana navyo. Kuongezea, walieleza kuwa vipengele vya kuzuia ushindani kikazi ni jambo la kawaida kwenye sekta ya kibinafsi ili kulinda maslahi ya halali na wala siyo hali isiyoleta haki kazini.

Bridge ilieleza kuwa tukio linalotajwa na Walalamishi, pale Bridge ilipeleka aliyewahi kuwa mwajiriwa mahakamani kwa kwenda kinyume na vipengele vya kuzuia ushindani ni kweli. Ilitokea hivi kwa sababu aliyewahi kuwa mwajiriwa alianzisha shule iliyoshindana na Bridge, hali iliyovunja sheria ya kulinda biashara dhidi ya ushindani. Kesi hiyo ya Bridge baadaye iliondolewa mahakamani.

*Matumizi ya kompyuta za walimu*

Bridge ilieleza kuwa walilenga kutumia njia za kufundisha zilizothibitishwa kuwa mwafaka ili kutoa elimu ya hali ya juu. Walisema kuwa matumizi ya kompyuta za walimu, ni muhimu ili kutoa elimu ya kiwango cha juu kwa sababu walimu huandaliwa vizuri ili kufundisha. Kompyuta za walimu huwezesha walimu kunufaika kutokana na vipindi vilivyopangiliwa vizuri kwa kiwango cha kimataifa kutokana na utafiti wa utaratibu wa kufundisha kwa njia bora zaidi. Bridge ilirejelea utafiti wa Benki ya Dunia na kueleza kuwa nchi maskini na zile zinazoendelea ambapo walimu hutatizika mara kwa mara kuelewa mada, walimu hupewa mwongozo kuwasaidia. Muda ambao walimu huokoa wakitumia andao la somo uliotayarishwa huwawezesha kutumia muda wao kufundisha wala siyo kupanga na kuendeleza vipindi. Bridge ilidokeza kuwa kompyuta za walimu husababisha mazingira mazuri darasani yanayoruhusu mwalimu kuingiliana na wanafunzi na mada zaidi. Hutokana na maoni ya watu waliotumia, zinajali wanafunzi na hufanikiwa kuwasaidia wanafunzi kusoma. Bridge ilisema kuwa, kwa kuwaondolea walimu jukumu la kuandaa vipindi, wanao uwezo wa kutumia muda huo kusaidia watoto wanaotatizika na kujumuika na wazazi.

Bridge iliendelea kwa kueleza kwamba kompyuta za walimu hutumiwa kote ulimwenguni na mashirika mengi yanayofanya kazi kwa nchi zaidi ya moja. Serikali ya Kenya, kwa ushirikiano na USAID hutumia kompyuta za walimu kuboresha elimu katika mradi wao wa TUSOME Kuwezesha Watoto wa Madarasa ya Chini kusoma na kuandika na MradI wa Kukuza Elimu ya Msingi (PRIEDE) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Bridge ilieleza CAO kuwa mfumo ulioandikwa unaotumiwa na Bridge umethibitishwa kufaulu Marekani kupunguza mwanya hadi nusu ulionyesha utofauti wa mafanikio kati ya wanafunzi wazungu na Waafrika.

Bridge pia ilirejelea ripoti za utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia na UWEZO, pamoja na mashirika mengine, na kueleza kuwa kutumia kompyuta za walimu iliwawezesha kukusanya data haraka inayoonyesha vipindi vilivyofanikishwa na vile vinavyopaswa kurudiwa. Pia huwasaidia kutambua walimu wanaohitaji msaada zaidi na pia kufuatilia na kuzuia walimu kukosa kwenda shuleni, hali iliyokithiri nchini Kenya.

Kwa kuongezea, Bridge ilisema kuwa kuongezwa wakati wa kufundisha hakufanyi hahuisi au kuwa kinyago au roboti kama walivyodai Walalamishi, lakini kuwa, sifa za kila mojawapo wa walimu na mtindo wao wa kufundishia hujitokeza hata wakitumia kompyuta za walimu. Bridge inaamini kuwa kompyuta za walimu ni njia ya kukuza uwezo wa walimu na kuwafanya kuwa bora zaidi, wanaojiamini na kujitolea kwa wanafunzi wao. Waliongeza kwamba kompyuta za walimu ziliundwa ili kuboresha maarifa na majukumu ya waunda vipindi na walimu kwa jumla. Watengenezaji wa vifaa vya kufundishia hutengeneza kwa makini jozi za matatizo ya kutatuliwa kwenye hesabu, na msusuru wa masuali ya kupima uelewa baada ya kusoma makala, kwa kuzingatia tafiti za hivi majuzi za mbinu mwafaka za kufundishia. Walimu huwa mstari wa mbele kuangalia na kushughulia kila mwanafunzi kutegemea wanavyofanya darasani.

*Kutafuta Wateja*

Bridge ilisema kuwa walimu walikuwa kwa nafasi bora kuelezea wazazi wapya na wanafunzi kuhusu madarasa ya Bridge yenye teknolojia na jinsi wanafunzi watakavyonufaika. Waliendelea kwa kusema kuwa ijapokuwa walimu wa shule za umma hawatarajiwi kufanya kazi wakati wa likizo, walimu wa shule za kibinafsi hawatarajii hali yao itakuwa hivyo. Bridge iliongeza kuwa, kwa mujibu wa sheria za kazi zinazotumika, wametenga muda wakati wa likizo ili walimu watafute wanafunzi na kufanya mambo mengine yanayowawezesha kujumuika na wazazi walioko na wazazi watarajiwa. Bridge hupanga kalenda yake kuhakikisha likizo ya walimu ya mara moja kwa mwaka haiathiriwi. Bridge ilisisitiza kuwa kinyume na hali ilivyo kwenye shule zingine kwenye jamii wanamofanya kazi, walilipa wafanyikazi wao mshahara kila mwezi mwakani, na siyo tu siku shule zinafanya kazi.

Zaidi ya hayo, Bridge ilidokeza kuwa, ijapokuwa kila mojawapo wa shule zake ilitakiwa kufikisha idadi fulani ya wanafunzi wageni kila mwaka, hakuna mwalimu aliyetakiwa kuwa ni yeye atakayehakikisha idadi hiyo inafikiwa kwa juhudi zake binafsi. Walimu wanapaswa kufanya kazi na meneja ili kupendekeza shule katika jamii. Wakati mwingine kuna utaratibu unaomwezesha mwalimu kupata kitu zaidi kwa kila mwanafunzi mgeni anayejiunga na shule ya Bridge na kulipa karo. Kwa mujibu wa Bridge, wao hutuza tu na wala hawatozi faini.

Kuhusiani na udhamini wa wanafunzi, Bridge ilisema kuwa wamo mbioni kutafuta wabia au wafadhili walio na matamanio ya kuwadhamini wanafunzi wao. Hata hivyo, walidokeza kuwa huwa hawawahakikishii wazazi kuwa watapata ufadhili. Iwapo Bridge wangepata malalamishi kuwa wafanyikazi wao wanaahidi udhamini, basi wangepeleleza kwa kuzingatia sera zao za kazi na kuchukua hatua mwafaka. Bridge ilijulisha CAO kuwa walikuwa na nambari ya simu na barua pepe inayoweza kutumiwa na wazazi kutoa malalamishi yao.

Bridge pia ilitoa stakabadhi zilizokuwa na ushahidi zaidi ya 1500 kutoka kwa walimu na wazazi walioonyesha kuridhika na Bridge ili kuunga mkono walisema.

### iii. Masuala yanayohusiana na mazingira ya shule

*Karo*

Bridge ilieleza kuwa nyingi ya shule zake zinapatikana kwa maeneo yanayokabiliwa na umaskini uliokithiri ambapo familia hutumia chini ya dola 2 kwa siku. Shule zake hutoa elimu ya kiwango cha juu kwa watoto kutoka kwa jamii maskini ambapo isingekuwa hivi pengine hawangepata elimu ya kiwango cha juu. Shule hizo hukamilishana na shule za serikali katika jamii maskini na hutoa njia mbadala ya masomo kwa shule za kibinafsi kwa familia kwa ada ya chini. Karo, kama ilivyoelezwa na Bridge, huchapishwa kwenye kila shule na ada ya wastani ni takribani dola 7 kwa mwezi na takribani dola 90.25 kwa mwaka. Hii imepungua kwa asilimia 40 ikilinganishwa na ile wastani ya shule zisizo rasmi zinazopatikana kwa jamii maskini. Bridge ilikanusha yaliyosemwa na Walalamishi kuwa karo huongezwa kila mwaka, bila kuwajulisha walimu na wazazi kwanza. Bridge ilidai kuwa ijapokuwa ni jambo la kawaida kwenye biashara kuongeza ada ya malipo kutokana na mfumuko wa bei na kuongezeka kwa bei ya bidhaa, Bridge haiongezi karo kila mwaka. Kuna miaka mingine ambapo hakuna kuongeza karo hata kama mfumuko wa bei umeongezeka au kupungua kwa asilimia 8 kwa miaka ya hivi majuzi. Walielezea pia kuwa hawakuongeza karo mwaka wa 2017 na eti katika mwaka wa 2019, kuna baadhi ya shule zilizopunguza karo. Kulingana na Bridge, wakati ambapo karo inaongezwa, uamuzi huo hufanywa kwa pamoja na shule, wazazi na Bodi ya Uongozi. Ongezeko hilo hutangazwa kwa muda wa karibu mwezi mmoja kabla ya mwaka mpya wa shule kuanza, na mara nyingi kabla ya kukamilika kwa mwaka uliotangulia.

Bridge ilisema pia kuwa, kinyume na inavyodhaniwa, shule za serikali si za bila malipo. Mara nyingi, wao hutoza karo ya kujiunga na shule, ada ya kuendeleza Muungano wa Wazazi na Walimu (PTA) na malipo mengineyo. Wazazi wanaopeleka wanao kwa shule za Bridge huchagua shule hizo wakiwa wanaelewa karo inayohitajika na hutumia hekima yao kufanya maamuzi kwa manufaa ya familia zao. Bridge iliongezea kuwa, kila wakati, kutakuwa na baadhi ya familia zisizokuwa na uwezo wa kulipa karo. Hata hivyo, hali hiyo haimanishi Bridge inabagua familia hizo. Walisema kuwa waliunda sera yao ya kulipa karo baada ya utafiti mpana na wamefundisha wasimamizi wao wa shule kutumia njia inayopendelewa na wazazi wakati wa kulipa karo. Badala ya kuitisha karo yote mara moja, Bridge huruhusu wazazi kulipa karo kidogokidogo muhula unapoendelea baada ya kujadiliana na meneja wa shule. Hii ni pamoja na kulipa kiasi kidogo kila mwezi. Kwa mujibu wa Bridge, utafiti uliofanywa miongoni mwa wazazi 380 mwaka wa 2017, ulionyesha kuwa asilimia 92 ya wazazi walioshiriki waliridhika na Bridge; asilimia 93 wanajivunia kuhusishwa na Bridge; na asilimia 83 wangependekezea rafiki shule hizo.

Bridge ilieleza kuwa bila kuwepo kwa shule za kibinafsi zisizokuwa rasmi katika jamii maskini, zaidi ya watoto milioni 2 wangesumbuka kupata elimu. Pia walisema kuwa, iwapo ingekuwa makosa kutoza karo kwa shule za kibinafsi, basi IFC haingewekeza katika taasisi za elimu za kibnafsi zinazotoza karo. Kinyume na hayo, IFC inahisi kuwa elimu kutoka taasisi za kibinafsi ni muhimu mno katika kusaidia taasisi za umma za elimu katika kutoa elimu ya chekechea, ya shule za msingi na ya shule za sekondari ili kuboresha elimu, na hivyo imefanya uwekezaji katika taasisi kadhaa zinginezo zinazolipisha karo nchini Kenya. Bridge ilisema kuwa wao, mara kwa mara, hutafuta watu binafsi na mashirika yanayoweza kusaidia wanafunzi wasio na uwezo wa kulipa karo. Kutokana na hali kuwa wao ni mojawapo wa shule chache zilizo na uwezo wa kutoa data ya kupatikana kwa walimu na wanafunzi darasani, wao huvutia wafadhili. Bridge ilielezea CAO kuwa EACHRights imesumbua wafadhili wake na kuwataka kusitisha ufadhili wao na kuwa hii ni kinyume na madai ya EACHRights kuwa wanataka kuona watoto wengi shuleni.

Bridge pia ilieleza kuwa malipo ya karo huwasaidia kujiendeleza, kulipa walimu, kulipia huduma za manispaa, kununua vitabu, na kukarabati miundo misingi shuleni. Kujiendeleza huku kunahakikisha kuwa wanafunzi kutoka familia maskini wanaendelea kupata elimu ya kiwango cha juu.

*Hali na Mahali Shule zinapatikana*

Bridge ilisema kuwa wao hutoa kwa wanafunzi wao mazingira salama ya kusomea. Shule zao zimejengwa kwa kutumia ramani za mijengo zilizoidhinishwa na serikali na kwa hivyo hufuata na kuweka sheria zinazotolewa na kitengo cha kanuni za elimu, Idara ya Kuhakikisha Ubora, na idara ya Afya ya Umma ya Kaunti. Shule hujengwa kutegemea hali ya anga, na kuhakikisha kuna mzunguko mzuri wa hewa na madirisha ya kutosha. Bridge ilisema kuwa wao hutekeleza mapendekezo yoyote yanayohitajika yanayotolewa na taasisi zitoazo sheria kila mara wanapoyapokea.

Kuhusiana na madai yanayohusu tatizo la usafi katika Kaunti ya Nyeri, Bridge walisema kuwa walikuwa na vifaa vya kutosha na mwafaka vya kuhakikisha usafi unadumishwa shuleni. Bridge ilieleza kuwa mojawapo ya kesi zilizopelekwa mahakamani katika Kaunti ya Nyeri ili shule ifungwe ilihusiana na shule kukaribiana na kichinjio. Mmiliki wa kichinjio alishindwa kukisafisha na kukiweka kwa hali safi kabla ya biashara hiyo kufungwa. Kutokana na hali hii, Idara ya Afya ya Umma ilitoa amri ya kufungwa kwa shule ya Bridge kwa misingi kuwa uchafu

kutoka kichinjioni ulikuwa kero na kusababisha uchafuzi wa mazingira ya shule. Bridge ilipeleka kesi mahakamani kupinga amri ya kufungwa kwa shule. Ombi lao lilitupiliwa mbali. Hata hivyo wahusika walipata suluhu nje ya korti.

Bridge pia ilieleza kuwa, kwa sababu nia yao ni kuwa na mazingira yaliyo salama kwa wanafunzi wao, wana mfumo wa kutatua matatizo ya usalama na kushughulikia usafi kupitia: Mfumo wa Kutunza Maslahi ya Wateja (CRM). Masuala ya usalama na usafi yanaweza kuripotiwa kwa Meneja wa Shule, kikosi cha Kuhakikisha Viwango vya juu, kikosi cha Maendeleo, na walimu na wafanyikazi wa Bridge. Malalamishi yanapotolewa, faili ya kuhakisha ukarabati unafanywa inafunguliwa. Ukarabati unapokamilika, Kikosi cha Kuhakikisha Ubora hufanya tathmini ya kazi iliyofanywa kuhakikisha kazi iliyofanywa imekidhi viwango vya usalama na/au usafi kabla ya faili kufungwa.

Wakizungumzia malalamishi yanayohusiana na hali ya viwanja vya shule, Bridge ilieleza kuwa huwahimiza Wakuu wa Shule washirikiane na wazazi na viongozi wa jamii kutunza viwanja vya shule. Juhudi hufanywa kudumisha usafi kwenye viwanja vya shule. Hata hivyo, wakati mwingine upepo mkubwa na mvua husababisha mafuriko na kusafirisha taka kutoka kwa vijiji hadi shuleni. Bridge ilieleza kuwa inasikitisha kwamba kuna wakati takataka huingia shuleni lakini wameweka mikakati ya kukabiliana na hali hii ikiwa ni pamoja na jinsi majengo yanavyojengwa, kuinua viwanja, kuchimba mitaro ili kupunguza athari za mafuriko kwenye viwanja vya kuchezea. Hata hivyo, haya ndiyo mazingira wanamofanyia kazi, na iwapo shule hazingeruhusiwa kufanyia kazi kwenye mazingira haya, wanafunzi hawangeenda shuleni.

Kwa mujibu wa Bridge haya maoni pia yalitolewa na mbunge aliyeshukuru Bridge kwa kazi wanayoifanya katika vijiji na akasema kuwa hakudhani ya kwamba ingewezekana kuwa na shule za aina hii katika jamii za aina hii. Bridge ilisema pia kuwa walikuwa na mikataba ya makubaliano kuwawezesha kutumia viwanja visivyokuwa na mijengo na kushiriki viwanja vya kuchezea na taasisi nyinginezo jinsi inavyodokezwa na serikali kupitia mwongozo wa APBET.

Bridge ilieleza kuwa majengo yao wakati mwingine huharibiwa na hali mbaya ya hewa. Katika Kaunti ya Nyeri, kuna shule ziliharibiwa kutokana na upepo mkali na mvua. Hali hii ilipelekea Idara ya Afya ya Umma kuwashitaki wafanyakazi wa Bridge. Hata hivyo, Bridge ilisema kuwa ilifanya ukarabati uliohitajika na kutathminiwa kwa ushirikiano wa Idara ya Afya ya Umma na Bridge. Ukaguzi ulionyesha kuwa Bridge iliridhia.

Wakizungumzia suala la vifaa vya kuwasaidia watoto wasiojiweza, Bridge ilisema kuwa shule zao zilijumuisha watoto wasiojiweza na pia kuwa, uhamasisho wao kuhusiana na suala hili umemulikwa na vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni pamoja na vya kitaifa na kimataifa. Bridge ilidokeza kuwa kama ilivyo katika shule nyingi nyinginezo, inakabiliwa na changamoto nyingi wakati wa kuwahudumia watoto wasiojiweza. Hata hivyo, walisema mafanikio yapatikanayo kwa watoto wasiojiweza katika shule za Bridge ni dhihirisho tosha la juhudi za Bridge za kuhakikisha watoto wasiojiweza kutoka jamii maskini wanapata elimu bora. Bridge pia ilieleza kuwa shule zake hazitambuliki kama shule za watoto wasiojiweza kwa mujibu wa kifungu cha 43 cha Sheria ya Elimu ya Msingi ya Kenya. Hata hivyo, hatua zilizochukuliwa kujumuisha watoto wasiojiweza kwenye shule hizo ni ishara tosha ya kujitolea kwao kuhakikisha watoto wote kutoka jamii maskini wanapata elimu bora.

Kuhusiana na utoaji wa nguvu za umeme, Bridge ilisema kuwa hakuna sheria ya kuhakikisha kuna stima kwa shule za mchana. Sheria inasema tu kuwa madarasa na majengo yanapaswa kuwa na mwangaza wa kutosha. Bridge ilisema kuwa walihakikisha kuwa madarasa yao yalipata mwangaza wa kutosha kwa kutumia mabati yanayopitisha mwangaza kwa madarasa yao yote. Hali inayowezesha kupatikana kwa mwangaza zaidi kupitia kwa paa mbali na ule wa kupitia kwa madirisha yao yanayoundwa wazi.

Kuhusiana na ua, Bridge ilisema ilitumia vitu mbalimbali vikiwemo waya, kuta za mawe, kuta za matofali, mabati, minyororo iliyounganishwa, na hukarabati nyua zao mara kwa mara. Kwa mujibu wa Bridge, maeneo ambayo kuna maduka ya pombe karibu na shule, wamelalamikia wanaohusika na uundaji wa sheria na mpangilio na wameweza kupata mafanikio kwa viwango mbalimbali.

Kuhusiana na vyoo, Bridge ilieleza wana utaratibu wa kukarabati na kuboresha vyoo mara kwa mara. Hii ni pamoja kuajiri watu wa kuviangalia, na kuhakikisha watu wa kutathmini kiwango cha ubora huviangalia mara kwa mara. Bridge pia ilieleza kuwa idadi ya vyoo kwa wasichana na wavulana kwa shule zao inarandana na matakwa ya Shirika la Afya Duniani (WHO). Mgawo hutokana na wastani wa idadi ya wavulana au wasichana wanaokuwa nje wakati wa vipindi vyao vya kupumzika, na wala siyo kutokana na idadi yao ya jumla shuleni. Bridge ilieleza kuwa huunda ratiba yake kuhakikisha kuwa wakati wa mapumziko hakuna wakati mgawo wa wanafunzi kwa choo watakuwa wengi nje wakitaka kutumia choo wakati wowote.

Wakizungumzia vifaa vya jikoni, Bridge ilieleza kuwa Bodi ya Uongozi, inayoteuliwa na wazazi, huhakikisha wanafunzi wanaweza kununua chakula cha mchana kilicho bora, salama na chenye virutubishi kwa bei ya chini kutoka kwa muuzaji binafsi aliye na cheti cha afya.

Hatimaye, wakizungumzia madai ya wanafunzi wengi darasani, Bridge ilisema kuwa hakuna sheria ya kudhibiti idadi ya mgao wa wanafunzi kwa walimu madarasani.

## 4. HATUA ZINAZOFUATA

Wakati wa mchakato wa kutathmini uliaofanywa na CAO, Bridge walionyesha utayari wa kushiriki katika mchakato wa kutatua mzozo kati yao na Walalamishi chini ya usaidizi wa CAO. Hata hivyo, Walalamishi walipendelea malalamishi yao yashughulikiwe na Kitengo cha Ridhaa cha CAO (CAO's Compliance function). Kutokana na kutokubaliana kuhusu njia itakotumika katika kutatua mzozo, isiyolazimishiwa mtu na inahitaji kushirikisha Kampuni na Walalamishi haswa, malalamishi yatapelekwa kwa kitengo cha Ridhaa cha CAO kutathmini utendakazi wa IFC wa kimazingira na kijamii kwa kuzingatia Kanuni za Utendakazi wa CAO.

**KIAMBATISHO A. UTARATIBU UNAFUATWA NA CAO KUSHUGHULIKIA MALALAMISHI**
Punde baada za CAO kutangaza kuwa malalamishi yanakubalika, CAO hufanya tathmini ya mwanzo. Nia ya tathmini ya CAO ni: (1) kubainisha masuala na malalamishi yanayotolewa na mlalamishi/walalamishi; (2) kutafuta taaarifa kutoka kwa washikadau wengine kupata maoni yao kuhisiana na hal hiyo; na (3) kuwasaidia washikadau kuelewa njia wanazoweza kutumia kutatua mzozo na kubainisha iwapo wangependa kushirikiana kutafuta suluhu kupitia Kitengo cha Kutatua Mizozo cha CAO, au iwapo kesi hiyo inapaswa kushughulikiwa upya na Kitengo cha Ridhaa cha CAO.

Kwa kuzingatia Mwongozo wa Utendaji Kazi wa CAO,[2] hatua zifuatazo hufuatwa ili kushughulikia malalamishi yalioopokelewa:

Hatua ya Kwanza: **Kukubali** kuwa malalamishi yamepokelewa**.**

Hatua ya Pili: **Kukubalika:** Kubainisha iwapo malalamishi yanakubalika kushughulikiwa na CAO (hii hufanyika kwa siku za kufanya kazi zisizozidi 15).

Hatua ya Tatu: **Tathmini ya CAO:** Kutathmini maswala yaliyoibuliwa na kuwasaidia washikadau kuelewa na kubainisha iwapo wangependa kushirikiana kupata suluhisho chini ya usaidizi wa kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo, au iwapo kesi hiyo inapaswa kushughulikiwa na kitengo cha Ridhaa cha CAO ili kuchunguza iwapo utaratibu wote wa kimazingira na kijamii unaotolewa na IFC's/MIGA umefuatwa kikamilifu. Mda wa kutathmini unaweza chukua siku za kufanya kazi zisizozidi 120.

Hatua ya Nne: **Kuwezesha usuluhishaji**: Iwapo wahusika watakubali kushirikiana kutatua mzozo, Kitengo cha CAO cha kutatua mizozo kitashiriki. Hatua za kutatua mzozo huzingatia au kufuata Mkataba wa Maafikiano na/au kutumia sheria zinazowekwa chini na kukubaliwa na makundi husika. Inawezahusisha kusaidiwa/upatanisho, kushirikiana kuatafuta ukweli, au njia yoyote itakayokubaliwa inayoweza kuleta suluhisho au kusaidia kufikia malengo yaliyowekwa kwa pamoja. Lengo kuu la kutumia njia hii kutatua mzozo ni kushughulikia wasuala yanayojitokeza kwenye malalamishi, na masuala mengine yoyote muhimu yanayohusiana na malalamishi yaliyojitokeza wakati wa kutathmini mzozo au wakati wa mchakato wa utatuzi kwa njia inayokubalika kwa wahusika wote[3].

AU

**Kutathmini kwa Ridhaa/Uchunguzi:** Iwapo wahusika watachagua mchakato wa kuridhia, kitengo cha CAO cha Ridhaa kitaanza kutathmini iwapo utaratibu wote wa kimazingira na kijamii unaotolewa na IFC's/MIGA umefuatwa kikamilifu kuhusiana na mradi husika. Hii itasaidia kubainisha iwapo uchunguzi wa utendakazi wa IFC/MIGA kuhusiana na mradi una mashiko. Mda wa kutathmini unaweza kuchukua mda usiozidi siku za kufanya kazi 45. Uchunguzi ukipatikana kuwa na mashiko, kitengo cha CAO cha Ridhaa kitafanya uchunguzi wa kina unaohusu utendakazi wa IFC/MIGA. Ripoti ya uchunguzi ikijumuisha mambo yoyote yanayoonyesha kutoridhia itawekwa wazi, pamoja na hatua zilizochukuliwa na IFC'/MIGA.

---

[2] Kwa maelezo Zaidi kuhusiana na majukumu na kazi ya CAO, tafadhali angalia kwa mwongozo mzima wa utendakazi kwenye: http://www.cao-ombudsman.org/documents/CAOOperationalGuidelines_2013.pdf

[3] Pale ambapo washikasau watashindwa kutatatua matatizo kwa ushiriakiano kwa mda uliowekwa, Kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo kitaanza kwa kujaribu kuwasaidia kukabiliana na changamoto. Iwapo haitawezekana, Kikosi cha kutatua mizozo kitawaeleza washikadau, wakiwemo wafanyikazi wa IFC/MIGA, Rais na bodi ya Benki ya Dunia, na umma kuwa, Kitengo cha CAO cha Utatuzi wa Mizozo kimefunga malalamishu na kuyahamishia kwa Kitengo cha Ridhaa cha CAO ili kutathminiwa.

Hatua ta tano: **Ufuatiliaji**

Hatua ya Sita: **Hitimisho/Kufungwa kwa kesi**